



CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO CHA HAZINA
HAZINA SAVING AND CREDIT COOPERATIVE SOCIETY LTD
Madaraka Avenue, P.O.BOX 9111, Dar Es Salaam Tel: 0710 933944,
0710606605 REG. No.DSR: 1822



Email: info@hazinasaccos.co.tz Website: www.hazinasaccos.co.tz

Kumb.Na.HSCS/05/2026

29/05/2026

TANGAZO LA KAZI ZA MAFUNZO KWA VITENDO (INTERNSHIP).

Nafasi: Afisa Mahusiano (Relationship Officer)

Eneo: MWANZA

Muda: Mwaka mmoja

Maelezo ya Nafasi:

Hazina SACCOS ni Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo chenye makao makuu yake Dar es Salaam chini ya ulezi wa **Katibu Mkuu Wizara ya Fedha**. Hazina SACCOS imekuwa nguzo muhimu ya kifedha kwa watumishi wa umma Tanzania bara. Kwa sasa ina wanachama zaidi ya **11,000** na rasilimali zaidi ya **TZS bilioni 50.6**, huku akiba na amana zikifikia bilioni 42.2 na mikopo iliyodaiwa bilioni 42.3. **Dhamira** yake ni kuwa Ushirika wa fedha wenye nguvu unaokidhi mahitaji ya wanachama kwa huduma na mazao bora, na **Dira** yake ni kulinda misingi ya ushirika kwa kutoa huduma zinazokidhi changamoto za wanachama kwa wakati na gharama nafuu.

Hazina SACCOS imefungua huduma (outlet) kanda ya ziwa kwenye ofisi za Halmashauri ya Ilemela mkoani Mwanza kwa ajili ya kuhudumia watumishi wa Umma wa kanda ya ziwa. Hivyo inahitaji vijana wenye nguvu na moyo wa kujituma kujifunza kazi.

Majukumu:

- Kutoa elimu ya ushirika wa akiba na mikopo kwa Watumishi
- Kusajili Wanachama wapya
- Kuhudumia Wanachama kulingana na maelekezo na matakwa ya ofisi
- Kutekeleza majukumu mengine kama atakavyoelekezwa na uongozi

Sifa zinazohitajika:

- Mhitimu wa chuo kikuu kinachotambulika na serikali kwenye masomo ya ushirika, fedha, masoko, mahusiano kwa umma na Uchumi.
- Uwezo wa kuwasiliana na watu kwa ufanisi.
- Mwenye haiba ya mwonekano na mwenye kujari watu.
- Mwenye kujiheshimu na kuheshimu wengine
- Mwepesi wa kujifunza na kuendana na mazingira.

- Mwenye uwezo wa kujenga urafiki na watu


Jinsi ya kuomba:

Tuma maelezo mafupi (CV/Resume) yako na barua ya maombi kuelezea shauku yako kwa nafasi hii kwa:

Email: info@hazinasaccos.co.tz

Tarehe ya Mwisho ya Maombi: 15/06/2026

Wako katika ujenzi wa Hazina Saccos


Dkt. Festo Mwaipaja,
Mtendaji Mkuu,
HAZINA SACCOS LTD

